

# **MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI CHA TAREHE**

**17/11/2021**

## **WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

- |                       |              |
|-----------------------|--------------|
| 1. KEDMON CHIPANYANGA | - MWENYEKITI |
| 2. CHAINA MASAMAKI    | - KATIBU     |
| 3. EDWARD J. MTURI    | - MJUMBE     |
| 4. JOSIAH P.SAOKE     | - MJUMBE     |

## **WAALIKWA.**

- |                         |                           |
|-------------------------|---------------------------|
| 1. ALFAXAD M. KIZINGA   | - KAIMU MWANASHERIA(W)    |
| 2. BHOKE CHACHA         | - KAIMU AFISA MIPANGO (W) |
| 3. DR. DEUSDEDIT KALASO | - MGANGA MKUU WA WILAYA   |
| 4. WUMBE HARUN          | - KAIMU MWEKA HAZINA (W)  |

## **SEKRETARIETI.**

1. ROBERT MAKENDO
2. PASCHAL SAMSON

## **AGENDA ZA KIKAO.**

1. Kufungua Kikao.
2. Kuthibitisha agenda.
3. Mapokezi ya fedha Tshs 1,671,872,380/= na kuwasilisha mgawanyo wa fedha kwa vyumba vya madarasa ya shule za msingi , sekondari, bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalum uchimbaji wa kisima kirefu na miundo mbinu ya kunawia mikono.
4. Mengineyo.
5. Kufunga kikao.

## **CTB/2021/2022/01: KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua kikao saa nne na nusu (04:30) asubuhi kwa kuwakaribisha wajumbe waliohudhuria na kuwaomba kuchangia kwa

umakini ili kuwezesha maombi yaliyo mbele ya kikao kuidhinishwa kutekelezwa haraka na kwa ufanisi kwa manufaa ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama.

**CTB/2021/2022/02: KUTHIBITISHA AGENDA.**

Jumla ya agenda tano zilisomwa na Katibu wa Bodi ya Zabuni na zikathibitishwa na kujadiliwa na wajumbe wote waliohudhuria katika kikao.

**CTB/2021/2022/03: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA TSHS 1,671,872,380/= NA KUWASILISHA MGAWANYO WA FEDHA KWA VYUMBA VYA MADARASA YA SHULE ZA MSINGI, SEKONDARI, BWENI LA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUM UCHIMBAJI WA KISIMA KIREFU NA MIUNDO MBINU YA KUNAWIA MIKONO.**

Katibu aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha jumla ya **Tshs 1,671,872,380/=** zikiwa na mchanganuo wa kutekeleza miradi ifuatayo.

1. Ujenzi wa vyumba 72 vya madarasa katika shule 19 za sekondari kiasi cha Tshs. 1,440,000,000/=
2. Ujenzi wa vyumba 6 vya madarasa katika shule shikizi za msingi 3 kiasi cha Tshs 120,000,000/=
3. Ujenzi wa bweni 1 la wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ya msingi Madaraka kiasi cha Tsh 80,000,000/=
4. Uchimbaji wa kisima kirefu na ujenzi miundo mbinu ya kunawia mikono katika shule ya msingi Nyamisisi kiasi cha tshs. 31,872,380/=

Wajumbe walipokea taarifa hiyo, baada ya kujadiliana kwa pamoja walilidhia miradi yote itekelezwe kwa kutumia njia ya manunuzi ya force account. Aidha pia walielekeza ununuzi wa saruji na tofali za miradi ya ujenzi vyumba 72 vya madarasa ya shule za sekondari ufanyike kwa pamoja (Bulky procurement).

**CTB/2021/2022/04: MENGINEYO.**

Hapakuwa na mengineyo

**CTB/2021/2022/05: KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti alifunga kikao saa sita na dakika thelethini (06:30) Alasiri kwa kuwashukuru wajumbe kwa usikivu walioonesha na mijadala mizuri waliyofanya kwa maslahi mapana ya Halmashauri.

**MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA:**

  
.....  
MWENYEKITI

  
.....  
KATIBU

.....  
30/12/2021  
TAREHE